

MWONGOZO KWA ANAYEKUSUDIA KUCHINJA MNYAMA WA UDH-HIYA

عن أم سلمة - رضي الله عنه - أن النبي صلوات الله عليه وآله وسلامه - قال: (إذا رأيتم هلال ذي الحجة وأراد أحدكم أن يضحي فليمسك عن شعره وأظفاره حتى يضحي) وفي رواية: (فلا يَمْسَّ من شعره وبشرته شيئاً) أخرجه مسلم (١).

الحديث دليل على أنه إذا دخلت العشر وأراد الإنسان أن يضحي فإنه لا يأخذ من شعره ولا من أظفاره ولا من بشرته شيئاً إلى أن يذبح أضحيته، فإن كان له أكثر من أضحية جاز له الأخذ بعد ذبح الأولى.

وأظهر قولي أهل العلم أن ذلك للتترحيم، لأنه الأصل في النهي، فإن تعمد وأخذ فعليه التوبة والاستغفار، ولا فدية عليه إجماعاً، ولا يؤثر ذلك على أضحيته.

وهذا النهي يخص صاحب الأضحية، لقوله: (وأراد أن يضحي) فلا يعم الزوجة ولا الأولاد إذا أراد أن يُشرِّكُهم معه في الثواب. ومن ضحي عن غيره بوصية أو وكالة فلا يحرم عليه أخذ شيء من شعره أو ظفره أو بشرته، لأن الأضحية ليست له. ومن أخذ من شعره المباح أخذها، أو ظفره أول العشر لعدم إرادته الأضحية ثم أرادها في أثناء العشر أمسك من حين الإرادة.

ومن احتاج إلى أخذ شيء من ذلك لتضرره ببقاءه كأنكسار ظفر أو جرح عليه شعر يتغير أخذه فلا بأس، لأن المضحي ليس بأعظم من الحرم الذي أبى له الحال إذا كان مريضاً أو به أذى من رأسه، لكن الحرم عليه الفدية والمضحي لا فدية عليه. (١) أخرجه مسلم (١٩٧٧). ولا يجوز للمرأة أن توكل أحداً على أضحيتها لتأخذ من شعرها - كما قد تفهمه بعض النساء - لأن الحكم متعلق بالمضحي نفسه سواء وكلَّ غيره أم لا، وأما الوكيل فلا يتعلق به نهي.

ولا حرج في غسل الرأس للرجل والمرأة أيام العشر، لأنه - إنما نهى عن الأخذ، ولأن الحرم أذن له أن يغسل رأسه.

المصدر: أحاديث عشر ذي الحجة و أيام التشريق أحكام وآداب ، عبدالله بن صالح الفوزان.

Kutoka kwa Ummu Salama Allah amridhie amesema; hakika

Mtume صلوات الله عليه وآله وسلامه amesema: ((Pindi mtakapoona mwezi mwandamo wa Dhulhijjah na mmojawenu akakusudia kuchinja mnyama wa udh-hiya basi asikate nywele zake na kucha zake mpaka atakapochinja)). Na ndani ya mapokezi mengine amesema ((Asikate chochote katika nywele zake wala sehemu ya ngozi yake)) Muslim.



adithi hii inajulisha kwamba hakika yanapoingia masiku kumi ya mwanzo katika mwezi wa Dhulhijjah, na mtu akawa anakusudia kuchinja mnyama wa udh-hiya **basi haitakiwi kunyoa chochote katika nywele zake wala kucha zake wala kukata sehemu ya ngozi yake, mpaka atakapochinja mnyama wake**. Endapo atakuwa na wanyama zaidi ya mmoja itafaa kunyoa na kukata kucha baada ya kumchinja mnyama wa kwanza.

Na dhahiri ya kauli mbili za wanachuoni ni kwamba, **katazo hilo la kunyoa na kukata kucha ni katazo la kuharamisha**, kwa sababu ndio asili ya katazo lolote la kisheria. Endapo atanyoa na kukata kucha kwa makusudi ni wajibu juu yake afanye toba na kuomba msamaha kwa Allah, na wala hakuna fidia yoyote itolewayo (kwa kosa hilo) kwa makubaliano ya wanachuoni wote. **Wala pia kosa hilo haliathiri chochote katika (usahihi na ukubalikaji wa) mnyama wake wa udh-hiya**.

Na katazo hili linamuhusu **mwenye mnyama (aliyekusudia kuchinja mnyama)** kwa kauli yake Mtume  aliposema ((..na akakusudia kuchinja mnyama wa udh-hiya)) , katazo hili halimuhusu mke wala watoto pindi atakapotaka kuwashirikisha katika thawabu za kuchinja. Na yelete ambaye **amechinja mnyama kwa ajili ya mtu mwengine kwa sababu ya kupewa usia au kumuwakilisha, si haramu kwake kunyoa au kukata kucha** kwa sababu mnyama huyo wa udh-hiya si wa kwake (bali yeye kape-wa usia kuwa amchinje fulani, au kakabidhiwa mnyama ili amchinje kwa kumuwakilisha mwenye mnyama huyo).

Na yelete ambaye **ameshakata kucha na kunyoa nywele baada ya kuingia mwanzo wa mwezi wa Dhulhijjah kwa sababu ya kuto-kusudia kuchinja, kisha baada ya hapo akakusudia kuchinja katikati ya masiku hayo kumi, basi atajizuia kukata kucha na kunyoa nywele kuanzia (siku) atapokusudia kuchinja.**

Na yelete atakayehitajia kukata kucha au kunyoa nywele kwa sababu ya kudhurika na ubakiasi wake, kama vile ukatikaji wa kucha (kwa kujikwaa n.k) au akapata jeraha juu ya nywele kiasi ambacho ikalazimika kutoa kucha iliyobaki au kutoa nywele (ili atibewe jeraha lake), basi hakuna tatizo kukata. Kwa sababu mchinchaji wa mnyama wa udh-hiya si mwenye taadhima zaidi kuliko mfanyakaji wa ibada ya Hija ambaye naye karuhusiwa kunyoa

endapo atakuwa ni mgonjwa au kukiwa na maudhi kichwani kwake ; isipokuwa mfanyakaji wa ibada ya Hija (endapo atanyoa kwa sababu hizo zilizoruhusiwa) ni wajibu juu yake atoe fidia , lakini aliyekusudia kuchinja mnyama wa udh-hiya (endapo atanyoa au kukata kucha kwa sababu ya udhuru wa kisheria) hana fidia yoyote iwajibikayo juu yake.

Na wala haifai mwanamke kumuweka mwakilishi wa kumchinjia mnyama wake wa udh-hiya ili mwanamke huyo anyoe nywele zake (au ili akate kucha zake); kama ambavyo inavyofahamika kwa baadhi ya wanawake. Kwa sababu hukumu ya uharamu wa kunyoa na kukata kucha inaambatana na mwenye mnyama sawasawa aweke mwakilishi wa kumchinjia au achinje mwenyewe. Ama mwakilishi aliyewekwa kwa ajili ya kumchinjia mtu mwengine, katazo hili halimuhusu.



ala **si vibaya kuosha nywele** kwa upande wa mwaname na mwanamke ndani ya masiku haya kumi, kwa sababu Mtume  amekataza kunyoa (au kupunguza) nywele tu (na wala hakukataza kuosha nywele), na kwa sababu (hata) mfanyakaji wa ibada ya Hija naye ameruhusiwa kuosha nywele zake.

والحكمة في هذا النهي . والله أعلم . أنه لما كان المضحي مشاركاً للمحرم في بعض أعمال النسك ، وهو التقرب إلى الله بذبح القرابان ، كان من الحكمة أن يعطي بعض أحكامه ، وقد قال الله في الحرمين : (وَلَا تَحْلِقُوا رُؤُسَكُمْ حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْهُنْدُي عَلَّهُ) (البقرة: 196) .

(تنبيه) : يتوجه بعض العامة أن من أراد الأضحية ثم أخذ من شعره أو ظفره أو بشرته شيئاً في أيام العشر؛ لم تقبل أضحيته، وهذا خطأ بين، فلا علاقة بين قبول الأضحية والأخذ مما ذكر، لكن من أخذ بدون عذر فقد خالف أمر النبي ﷺ بالإمساك، ووقع فيما نهى عنه من الأخذ، فعليه أن يستغفر الله ويتبوب إليه ولا يعود، وأما أضحيته فلا يمنع قبولها أخذه من ذلك.

وأما من احتاج إلى أخذ الشعر والظفر والبشرة فأخذها فلا حرج عليه، مثل أن يكون به جرح فيحتاج إلى قص الشعر عنه، أو ينكسر ظفره فيؤديه فيقص ما يتآذى به، أو تتدلى قشرة من جلدته فنؤديه فيقصها، فلا حرج عليه في ذلك كله.

المصدر: أحكام الأضحية والذكرة للعشرين رحمة الله تعالى

Na hekima ya katazo hili la kunyoa na kukata kucha ni kwamba; kwa kuwa mchinjaji wa udh-hiya anashirikiana (anafanana) na mfanyaji wa ibada ya Hija katika baadhi ya matendo ya ibada hiyo kama vile kujisogeza kwa Allah kwa kufanya ibada ya kuchinja, imekuwa ni hekima apewe baadhi ya hukumu zake (yaani apewe hukumu za mfanyaji wa ibada ya Hija ikiwemo uharamu wa kukata kucha na kunyoa nywele) kama alivyosema Allah Mtukufu kuhusu wafanyaji wa ibada ya Hija ((Na wala msinyoئe nywele zenu mpaka mtakapochinja)) Albaqara 196 ; na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Uzindushi:

Baadhi ya watu wasiojua wanadhani kwamba atakayekusudia kuchinja mnyama wa udh-hiya kisha akakata kucha zake au akanyoa nywele zake au akakata sehemu yoyote ya ngozi ya mwili wake ndani ya masiku haya kumi, uchinjaji wake wa udh-hiya haukulaliki (si sahihi), na dhana hii ni makosa ya wazi kwa sababu hakuna uhusiano wowote kati ya kukulalika mnyama wa udh-hiya na ukataji wa kucha au unyoaji wa nywele. Lakini yeyote atakayekata kucha au kunyoa nywele pasina udhuru wowote wa kisheria anakuwa amepingana na amri ya Mtume ﷺ ya kujizua kutokata na kutonyoa, na anakuwa ameingia katika jambo ambalo Mtume amelikataza, hivyo ni wajibu juu yake afanye toba na aombe msamaha kwa Allah Mtukufu.

Ama Yule ambaye atahitajia kunyoa nywele au kukata kucha zake au kukata shemu ya ngozi ya mwili wake , akafanya hivyo (kwa dharura) hakuna tatizo juu yake. **Mfano akawa na jeraha akahitajia kupunguza nywele katika jeraha hilo, au kucha ikakatika yenewe (ikawa inaning'inia) ikawa inamuudhi na kumsumbuu akawa amekata kipande cha kucha inayomuudhi, au kipande cha ngozi ya mwili kikawa kinaning'inia na kikawa kinamuudhi, akakikata; hakuna tatizo lolote katika hali zote hizo.**

وصلى الله على محمد وآلـه وصحبه وسلم

Mkusanyaji na Mkalimani: Ummati Abdallah, Abuu Muhammad